

**HOTUBA YA MHE. JAJI MKUU KATIKA HAFLA YA KUTAMBUA
MICHANGO YA WADAU KATIKA MATUMIZI YA NJIA MBADALA
YA USULUHISHI TAREHE 16 JANUARI, 2024 KATIKA UKUMBI
WA MWL. NYERERE, JNICC.**

Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani mliopo,

Mhe. Zahra Maruma, Jaji Mfawidhi, Kituo cha Usuluhishi,
Mahakama Kuu,

Wahe. Majaji Wafawidhi wote mliopo,

Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu mliopo,

Wahe. Majaji Wastaafu mliopo,

Mhe. Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama,

Mhe. Sylvester Kainda, Msajili wa Mahakama ya Rufani na Kaimu
Msajili Mkuu,

Wahe. Makatibu Wakuu wote mliopo,

Mhe. Projestus Kahyoza, Kaimu Msajili Mahakama Kuu,

Watendaji wote wa Mahakama Kuu na Divisheni zote,

Dkt. Boniface Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali,

Wahe. Naibu Wasajili wote mliopo,

Wahe. Mahakamu wote mliopo,

Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Mabaraza mbalimbali mliopo,

Wawakilishi wote wa Taasisi za Kiserikali na Binafsi mliopo hapa,

Wakurugenzi wote wa Taasisi za kifedha mliopo,

Wageni wote waalikwa,

Ndugu Waandishi wa Habari mliopo,

Mabibi na Mabwana,

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Mahakama ya Tanzania!

1. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuuona mwaka 2024. Niwatakie nyote Heri ya Mwaka Mpya.

Pili, kwa niaba ya Mahakama ya Tanzania, ninapenda kushukuru Kituo cha Usuluhishi kwa kuandaa na kunialika katika hafla hii ya kutambua michango ya wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Mahakama katika Utatuzi wa Migogoro ya Madai kwa njia mbadala na pia kuzindua **Taarifa ya Utafiti wa**

Matumizi ya Njia Mbadala za Utatuzi wa Migogoro kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

2. Aidha, nichukue fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao mmeona umuhimu wa kuhudhuria tukio hili katika jitihada za kuhamasisha matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro. Na pia kutambua ushirikiano wenu katika kufanikisha tukio hili la kwanza na la aina yake kufanyika katika Kituo hiki cha Usuluhishi. Ninawaomba muendeleo kuona umuhimu wa kuendeleza jambo hili muhimu kwa nyakati zijazo.

3. Kama ilivyoelezwa na Jaji Mfawidhi wa Kituo cha Usuluhishi katika neno la utangulizi na pia katika barua zenu za mialiko, hafla hii inalenga kuwatambua na kuwapa tuzo Wadau wote wa Mahakama waliofanikisha matokeo mazuri katika usuluhishi kwa kipindi kilichopita. Kila mdau kwa namna moja au nyingine ameweza kuchangia kwa namna ya kipekee katika kuleta matokeo chanya na pia kutoa fursa kwa wananchi kufahamu njia sahihi ya usuluhishi wa migogoro yao pasipo

kwenda Mahakamani na kutokubali migogoro yao kuendelea kuwepo mahakamani kwa muda mrefu. Wakati tukiendelea kujumuika pamoja kwenye hafla hii fupi, hebu tuchukue wasaa wa kutafakari umuhimu wa mafanikio haya. Hafla hii muhimu inaongozwa na kauli mbiu isemayo “*KWA NINI SIO UPATANISHI*” [Why not mediation- a a strategic tool resolve civil disputes. Kauli mbiu hii ni mwendelezo wa kauli mbiu ya Siku ya Sheria ya mwaka, 2023 isemayo; **“UMUHIMU WA UTATUZI WA MIGOGORO KWA NJIA YA USULUHISHI KATIKA KUKUZA UCHUMI ENDELEU: WAJIBU WA MAHAKAMA NA WADAU”**. Kauli hii inaitaka Mahakama na Wadau kujielekeza zaidi katika matumizi ya njia mbadala katika kutatua migogoro ili kunufaika na faida za matumizi ya upatanishi (*Mediation*), usuluhishi (*Arbitration*), mazungumzo kufikia makubaliano (*Negotiation*) pamoja na kurudisha mahusiano ya kirafiki (*Conciliation*). Matumizi ya njia hizi mbadala uharakisha upatikanaji wa haki kwa haraka na kwa watu wote, huokoa muda na gharama za wadaawa ambazo zinaweza kutumika katika uzalishaji wa uchumi. Pia njia hizi mbadala zina faida nyingine kubwa kama vile ushiriki wa wenye mgogoro katika

kutafufa suluhu wao wenyewe, kuwepo kwa usiri na faragha kwa wadaawa, kutumia njia zisizo na utaratibu mgumu ambazo hukubalika kwa pande zote mbili pamoja na kuhifadhi mahusiano baina ya wadaawa.

4. Naomba nichukue fursa hii kuwapongeza wote watakaopewa tuzo leo kwa juhudi zenu za kufanikisha utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala na pia niwapongeze kwa heshima hii mliyopewa. Washiriki hawa wanaopewa Tuzo leo, wanatambuliwa na Kituo hiki kwa juhudi zao na mchango wao kwa kuiishi kauli mbiu inayosisitiza wadau wa Mahakama kuendeleza UTATUZI WA MIGOGORO KWA NJIA YA USULUHISHI ILI KUKUZA UCHUMI ENDELEVU. Kwa umuhimu wa pekee, nawapongeza pia Viongozi na Watumishi wote wa Kituo cha Usuluhishi kwa ubunifu wenu na uthubutu wa kuandaa tukio kama hili pamoja na changamoto zake katika kuanzisha jambo jipya kama hili. Ni imani yangu kuwa huu ni mwanzo wa mikakati yenu mkishirikiana na wadau katika kufanikisha matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro. Niwaombe muendelee kupanua wigo wa washiriki ili Tuzo kama

hizi ziunganishe nguvu za wadau wote kwenye eneo hili la usuluhishi. Aidha, naamini kuwa Tuzo hizo sio tu ni ishara ya kutambuliwa (*recognition*) na wala hazitaishia katika kuwatambua wadau hawa bali zitaendelea kuwa chachu za kuhamasisha kila mmoja wetu na jamii kwa ujumla kuona umuhimu wa kuendelea kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi.

5. Mwaka huu 2024, ni mwaka unaotupeleka katika kukamilisha robo ya kwanza ya Karne ya 21 mwishoni mwa Desemba, 2025. Sote tunafahamu kuwa mabadiliko makubwa yanayotokea katika Karne ya 21 yanayolazimisha Mifumo ya Sheria na ile ya Utoaji Haki ifanyiwe maboresho makubwa ili ilingane na kasi ya mahitaji ya karne ya 21. Kwa mujibu wa Dira 2025 – Karne ya 21 ni ya ushindani migogoro inapochelewa kukamilika Mahakamani – inapoteza ushindani. Lazima tutafakari kuwa sheria mbalimbali tunazotumia sasa hivi katika upatanishi na katika utatuzi wa migogoro bado zimejaa majoho na maudhui ya Karne ya 19 au 20. Ni wajibu wetu sasa ni kuhakikisha kuwa taratibu za kimahakama kuhusu utatuzi wa migogoro

zinalengewa misukosuko ya ushindani kwa kutumia njia mbadala za kutatua migogoro katika karne ya 21.

6. Ni sisi wadau ndio tutafanikisha matumizi ya Teknolojia katika eneo la usuluhishi. Tukumbuke kuwa tayari Teknolojia inatumika kufungua mashauri kwa njia ya mtandao (*e-filing*), katika ugunduzi wa kielektroniki (*e-discovery*), katika matumizi ya huduma ya mifumo ya unukuzi na tafsiri (*real time transcription and translation services*), katika matumizi ya video-links, na maeneo mengine mengi ya usuluhishi.

7. Tukubaliane kuwa watakaofanikisha maboresho kwa kupitia matumizi ya usuluhishi kutatua migogoro sio wengine bali ni Mahakama na Wadau wa Mahakama katika mnyororo na mitiririko ya utoaji haki. Tuwaelimisha wadaawa na wananchi kuhusu faida kubwa inayopatikana kutoka katika usuluhishi wa migogoro kwa njia mbadala. Tuwakumbushe muda unaopotea kwa wadaawa kupitisha migogoro yao katika ngazi za Mahakama na hatua nyingi za kimahakama hadi kusubiri hukumu.

8. Tuhimize faida kubwa ikiwemo kupungua kwa gharama, kuokoa muda na kuharakisha ukamilishaji wa mashauri. Bado hapa nchini kwetu matumizi ya njia ya upatanishi katika utatuzi wa migogoro hazijaonyesha mafanikio kwa kiwango kikubwa. Hali hii pia inajidhirisha katika taarifa ya matumizi ya njia mbadala ya upatanishi iliyoandaliwa na Kituo cha Usuluhishi baada ya utafiti mdogo wa utekelezaji wa kauli mbiu ya siku ya sheria kwa mwaka 2023 kwa upande wa Mahakama pamoja na wadau wa Mahakama ambao wanashughulika na utatuzi wa migogoro kwa njia ya upatanishi katika mkoa wa Dar es salaam.

9. Tukiweza kuweka juhudi za pamoja katika kuimarisha matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro tutaweza kufanikisha malengo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) ya kutochelewesha haki bila sababu ya kimsingi [Ibara ya 107A (2) (b)]; kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro [Ibara ya 107A (2) (d)]; na kutenda haki bila kufungwa kupita kiasi na

masharti ya kiufundi yanayoweza kukwamisha haki kutendeka [Ibara ya 107A (2) (e)].

10. Upatanishi kwa sasa ni njia ya amani na inakubalika hata kimataifa ili kutatua migogoro. Matumizi ya Usuluhishi yanafaida kubwa ya kupandisha hadhi na nafasi ya Tanzania katika RIPOTI YA HALI YA UWEKEZAJI urahisi wa kufanya biashara inayoweka viwango vya kimataifa katika upimaji wa mfumo wa ushughulikiaji wa migogoro ya madai (*Civil Justice System*) ambapo nafasi ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya upatanishi bado ni wa chini sana na hautoi fursa kwa wawekezaji wa nje.

11. Ni matarajio yangu, kupitia hafla hii, changamoto zinazokwamisha kasi ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi zitaondolewa. Sote tutambue usuluhishi ni dhana yenye kututaka tubadili fikra zetu za utoaji haki zilizojengwa na mfumo wa utaoji haki unaochukua muda mrefu kabla ya mgogoro kumalizika kwa kufuata ngazi za kimahakama kuanzia mahakama za mwanzo hadi ya rufani, na kupitia

katika hatua nyingi, maahirisho mengi na mapingamizi mengi ya kiufundi ndani ya kila ngazi za Mahakama.

12. Kama nilivyogusia awali, Tanzania sio kisiwa katika kutekeleza azma ya kwenda sambamba na matumizi ya Teknolojia Mahakamani. Kituo cha Usuluhishi hakijabaki nyuma katika matumizi ya Teknolojias. Kituo hiki kimeendelea kutoa huduma ya upatanishi kupitia Mkutano Mtandao (*Video Conference and Video calls*). Kituo kimejipanga kutoa huduma za Usuluhishi Mtandao (*Online Mediation*) ambapo wadaawa hawalazimiki kufika kituoni ili kuhudhuria vikao vya upatanishi kupitia njia ya mtandao kwa viunganishi (*link*) maalum watakazopatiwa, naamini mawakili wanaopata huduma katika Kituo cha Usuluhishi wana uzoefu mzuri wa matumizi haya ya usuluhishi mtandao. Hivyo niwaalike wadau wa Mahakama kuweza kutumia njia hii katika usuluhishi wa migogoro mbalimbali bila kujali gharama na umbali.

13. Hivi sasa Mahakama ya Tanzania imeanza kutekeleza mpango wa kimaboresho wa kudijiti nyaraka zote za mahakama

(Digitization of court records). Huko ndiko wadau wote wa Mahakama katika mfumo wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi tunatakiwa kwa pamoja kuelekea, tufikie hatua za kudijiti.

14. Ripoti ya Tume Rais, iliyoangalia jinsi ya kuboresha taasisi za haki jinai nchini imetoa mapendekezo ambayo ni muhimu pia kwa taasisi za Haki Madai nchini. Kwa mfano, Tume ya Rais iliona changamoto ya mfumo ya TEHAMA kutosomana baina ya Taasisi za Haki Jinai, ukosefu wa miundombinu na ukosefu wa wataalam, upungufu wa vitendea kazi vya kisasa ambayo huchangia ucheleweshaji wa mashauri ya Jinai. Changamoto hizo ni muhimu kutafutiwa ufumbuzi na Taasisi za Haki Madai. Mifumo ya Teknolojia miongoni mwa wadau mliohudhuria hapa na wengine, ni lazima isomane ili tufikie azma yetu ya kumaliza migogoro mingi ya madai kwa njia ya usuluhishi.

15. Kwa kupitia hafla hii ni dhahiri tumepata kuelimika na faida za usuluhishi ambazo zina mchango mkubwa sana katika kukuza uchumi endelevu katika Taifa letu. Hivyo ni wajibu wa

Majaji, Mahakimu, Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea ambao ni wadau wa Mahakama; kila mara kuwakumbusha wadaawa uwepo wa hiyo nafasi ya kutatua migogoro nje ya Mahakama kwa kuwa kupitia utaratibu wa njia za usuluhishi ili wadaawa au pande mbili zenye mgogoro hupata fursa ya kukaa pamoja na kuzungumza, kuibua viini vya mgogoro, kujadili na hatimaye kufikia makubaliano ya kumaliza tofauti zao kwa ridhaa zao wenyewe.

16. Tunapohitimisha kauli mbiu ya SIKU NA WIKI YA SHERIA ya mwaka jana 2023, ni wito wangu kwa Mahakama, wadau wa Mahakama, wadaawa na wananchi kwa ujumla; kutatua migogoro kwa makubaliano au usuluhishi bila ya kupoteza muda na gharama pamoja na hatua ndefu za kimahakama hadi kusubiri hukumu.

17. Nichukue nafasi hii tena kukipongeza tena Kituo cha Usuluhishi kwa kuona umuhimu wa kutambua mchango wa wadau mbalimbali katika utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi. Jambo hili litaleta tija na hamasa kwa Mhimili wa

Mahakama pamoja na wadau katika kufikia malengo ya Mkakati wetu.

18. Kwa maneno haya nimalize kwa kuwapongeza na kuwashukuru tena wadau mbalimbali na pia Viongozi na Watumishi wote wa Kituo cha Usuluhishi kwa kushiriki katika tukio hili muhimu ambalo siyo tu linaboresha Usuluhishi nchini bali ni chachu ya Utatuzi wa Migogoro ya Madai kwa njia mbadala na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi katika Taifa letu kwa ujumla.

19. Baada ya kusema hayo, sasa niko tayari kuwatambua wadau wa ndani na wa nje ya Mahakama kwa kuwakabidhi tuzo za kutambua michango yao mbalimbali katika matumizi ya njia mbadala ya usuluhishi.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA!